

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

Anwani ya simu: "MAKAMU",
Simu Na.: +(255)026 2329006
Nukushi.: +(255)026 2329007/2983150
Barua Pepe: km@vpo.go.tz



Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
S. L. P. 2502,
40406 DODOMA,
TANZANIA.

Budapest - Hungary

13 Septemba 2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango leo tarehe 13 Septemba 2023 amewasili Jijini Budapest nchini Hungary ambapo anatarajia kumwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Tano wa Idadi ya Watu (*5th Budapest Demographic Summit*) utakaofanyika tarehe 14-15 Septemba 2023.

Mkutano huo wa siku mbili wenye kauli mbiu ya "Dhima ya Familia: *Msingi wa Usalama*" utahudhuriwa na Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka mataifa mbalimbali, Watunga Sera, Viongozi wa Taasisi na Mashirika ya Kimataifa, Viongozi wa Dini na Wanataaluma.

Pia Mkutano huo unatarajia kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi baina ya mataifa, uhaulishaji wa teknolojia na uvumbuzi pamoja na ushirikiano katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za maendeleo.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Franco Singaile'.

Franco Singaile
Msaidizi wa Makamu wa Rais - Habari